# STANDARD 5 MID TERM 2 EXAM 2019

## KISWAHILI

0052019 Muda: Saa 1 Dakika 40

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nambari 1 hadi 15 zilizoachwa wazi. Kwa kila nafasi, jaza kwa jibu sahihi.*

Vyakula vyenye sukari nyingi ______1_____ afya . Sukari husababisha _____2_____ wa meno hasa ___3___mswaki _____4_____ kuitumia. Mafuta mengi ni chanzo cha shinikizo _____5_____ damu, maradhi ya moyo na ini. Tunahitaji kubadilisha mwenendo wetu wa _____6_____ na kufuata ulio mzuri wa _____7_____. Kwa mtoto mchanga, maziwa ya mama yana virutubishi ______8______ vinavyohitajika ili mtoto ______9______ vyema.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. A. inadhuru | B. hudhuru | C. huimarisha | D. hukuza |
| 2. A. uozo | B. uhondo | C. upotevu | D. ugumu |
| 3. A. ukipiga | B. unapiga | C. usipopiga | D. unapopiga |
| 4. A. kabla ya | B. mwanzoni mwa | C. mbele ya | D. baada ya |
| 5. A. ya | B. za | C. pa | D. la |
| 6. A. makazi | B. ulaji | C. mazoezi | D. mavazi |
| 7. A. lishe sawa | B. milo sawa | C. lishe bora | D. vyakula vitamu |
| 8. A. kemkemu | B. kemukemu | C. haba | D. hapa |
| 9. A. akue | B. akuwe | C. avie | D. awe |

Hapo zamani za kale, chui na mbuzi walikuwa marafiki wa chanda na _____10_____. Walitekeleza _____11_____ zao pamoja kwa maelewano makubwa. Muda si muda mbuzi akawapata vimeme naye chui _____12_____. Waliwalea watoto wao kwa tunu na _____13_____ na kuwapa _____14_____ walichohitaji. Katika mambo yote, walishirikiana mfano wa _____15_____

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10. A. pete | B. kidole | C. mpenzi | D. kidani |
| 11. A. mambo | B. matembezi | C. shughuli | D. biashara |
| 12. A. shibli | B. visui | C. vidanga | D. vituju |
| 13. A. furaha | B. zawadi | C. sherehe | D. tamasha |
| 14. A. chochote | B.lolote | C. yoyote | D. yeyote |
| 15. A. maji na mafuta | B. mbingu na ardhi | C. uta na upote | D. pua na mdomo |



Compiled & supplied by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.***

**16.** Ni neno gani ambalo **lisilostahili** hapa?
A. Kochu B. Foronya
C. Fyekeo D. Zulia

**17.** Kipi ni kinyume cha:
**Alisimama mwangazani karibu na mzee?**
A. Aliketi nuruni mbali na ajuza.
B. Aliketi gizani mbali na kijana.
C. Aliketi gizani karibu na kijana.
D. Aliketi gizani mbali na mama.

**18.** Kutengana ni kwa mbingu na ardhi iihali kushirikiana ni kwa
A. pua na mdomo.
B. kinu na mchi.
C. maji na mafuta.
D. nyuki na mzinga.

**19.** Tambua sentensi ambayo imetumia tashbihi
A. Jitu lenyewe lilikuwa refu kama mlingoti.
B. Mto wenye mamba wakubwa ni huo.
C. Kiberenge ni swala, hakuna wa kumpiku.
D. Tulipowaona tulilia machozi ya bahari.

**20.** Ajali hiyo ilipotokea, aliponea
A. chuchupu.
B. chapuchapu.
C. chopi.
D. chupu chupu.

**21.** Kanusha :
**Nilienda hospitalini nikampata**
A. Sikuenda hospitalini nikampata.
B. Nilienda hospitalini sikumpata.
C. Sikumpata hospitalini nilipokwenda.
D. Sijakwenda hospitalini nikampata.

**22.** Vazi **lisilo** la kiume ni
A. koti B. kanchiri
C. bombo D. suruali

**23.** Tambua orodha ambayo imeambatanishwa **visivyo.**
A. Konokono - kombe
B. Samaki - maji
C. Nyuki - jana
**D. Ndege - kiota**

**24.** Tambua kundi la sauti za Kiswahili pekee
A. c, ny, ng' B. k, l, x
C. th, a, ma D. dh, n, z

**25.** Ni neno gani ambalo maendelezo yake yamekosewa?
A. Ghorofa
B. Sherehani
C. Kusheherekea
D. Kutumbuiza

**26.** **<u>Mvunguni</u> mwa kitanda mna panya**
Neno lililopigiwa kistari ni
A. nomino B. kitenzi
C. kihusishi D. kivumishi

**27.** Umbo hili la hilali ni la



A. mwezi mwandamano
B. mzinga
C. wavu
D. mlango

**28.** Ni sentensi gani iliyo sahihi kisarufi?
A. Walioingia katika darasani ni wengi.
B. Maziwa chafu ni hatari kwa afya.
C. Manyani wenye pua ndefu ni weusi.
D. Wenye walichelewa wote walifukuzwa.

**29.** Ikiwa leo ni Jumatatu, kesho kutwa itakuwa
A. Jumapili B. Jumanne
C .Jumamosi D. Jumatano

**30.** Kitendawili :
Likitoka halirudi.
A. Jua
B. Jani
C. Mwiba
D. Nuru

Compiled & supplied by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Ulimwengu wa karne ya sasa umeingia katika kipindi cha maendeleo ya hali ya juu katika uvumbuzi. Utafiti wa sayansi umeboreka nayo teknolojia inaongezeka . Teknolojia imeleta uvumbuzi wa tarakilishi, simu tamba, barua pepe na mengine ya kustajabisha. Mambo hayo ndiyo yameufanya ulimwengu kuwa katika hali iitwayo utandawazi. Ulimwengu umekuwa kama kijiji kidogo. Wengine wasiopenda kuuita utandawazi wao huuita utandaridhi. Hii ni ile hali ambapo mawasiliano yamekua kwa wepesi mno.

Sayansi katika kilimo imeleta maajabu yake. Si ajabu kumwona kuku asiye na haja na jogoo lakini bado anataga mayai. Mayai hayo huangua bila kuatamiwa. Chakula na dawa vinatosha kumfanya kuku atage mayai hayo. Kuku wanaofugwa kwa ajili ya nyama nao huwa tayari kwa kuliwa au **kupigwa bei** wafikapo hata umri wa wiki nane.

Mashine na mitambo mbali mbali zinatumiwa kurahisisha shughuli za kilimo. Si ajabu kuliona tingatinga moja likifanya kazi zote shambani. Tingatinga hilo litavuna nafaka, lichuje, litie kwenye magunia na hatimaye lishone magunia hayo, Kwa kutumia uvumbuzi wa sayansi mwanadamu ameniudu kuongeza mazao yake shambani na hata kuyaboresha. Utafiti imewezesha mimea , na matunda kukua na kupevuka kwa muda mfupi zaidi. Hivi karibu ukosefu wa chakula utazikwa katika kaburi la sahau.

**31.** Katika aya ya kwanza, mwandishi anaisifu karne ya leo kwa
A. uvumbuzi wa binadamu
B. maendeleo mengi
C. uvumbuzi wa hali ya juu
D. utafiti mwingi

**32.** Kulingana na kifungu ulichokisoma, teknolojia **haijaleta** uvumbuzi wa
A. rununu
B. barua pepe
C. kompyuta
D. ngoma

**33.** Hali ambapo dunia imekuwa kama kijiji kidogo kutokana na wepesi wa mawasiliano ni
A. teknolojia
B. utandaridhi
C. mawasiliano
D. kijiji

**34.** Kutokana na sayansi ya kisasa, leo inawezekana
A. mayai kuangua bila kuatamiwa
B. kuku kuatamia mayai bila kuangua
C. mayai kuatamiwa bila kuangua
D. kuku kutaga mayai

**35.** Mwandishi anasema kuwa kuku wa wiki nane pekee wanaweza kuwa nyama au
A. kutaga mayai
B. kuuzwa
C. kuatamia mayai
D. kuwa chakula

**36.** Ufugaji wa kuku na ulimaji wa mimea zote ni shughuli za
A. teknolojia B. kilimo
C. ziara D. kisasa

**37.** Tingatinga kwa mujibu wa kifungu, halina nafasi ya
A. uvunaji
B. uchujaji wa nafaka
C. upanzi
D. ushonaji wa magunia yenye nafaka

**38.** Kulingana na mwandishi, manufaa ya teknolojia ni
A. ongezeko la mayai
B. kuku wasiohitaji jogoo
C. tingatinga lenye shughuli nyingi
D. ongezeko la mazao shambani

**39.** Ikiwa matunda yatapevuka kwa muda mfupi zaidi, tunaweza kusema
A. itakuwa hasara kwa mkulima
B. chakula kitakuwa si haba
C. mkulima atafaidika zaidi
D. kila mtu atafurahia

**40.** Kutoka katika ufahamu tambua neno ambalo lina maana ya " uchunguzi wa kisayansi"
A. Utafiti
B. Uvumbuzi
C. Mashine
D. Teknolojia



Compiled & supplied by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Hapo zamani za kale paliondokea Simba ambaye alijitosa katika safari za kila siku za kuwasaka wanyama ili apate mlo. Alizunguka huku na kule lakini akashindwa kumpata mnyama yeyote; wanyama walijificha walipomwona. Basi alianza kurudi yalipokuwa makao yake makuu huku amejiinamia kwa huzuni na unyonge wa kukosa chakula. Kwa bahati nzuri alikutana na Panya aliyekuwa akijiendea zake. Simba aliamua kumkamata na kumla ili kukidhi njaa yake.

"Mimi nimekosa chakula kwa hivyo nitakumeza wewe Panya," alisema Simba kwa sauti nzito. Panya alimwangalia Simba kwa huruma kisha kwa sauti ya unyonge akasema "Sasa simba ukinila utafaidi na nini na mwili wangu ni mdogo siwezi hata kutoshea kwenye magego yako. Naomba uniachilie niende zangu, labda siku moja nitaweza kukulipa kwa fadhila yako hii," alisema Panya. Simba aliangua kicheko kikubwa na kusema, "Sasa mnyama mdogo kama wewe utanifaa kwa nini? Lakini haidhuru nitakuachilia uende zako."Simba alijiendea zake naye Panya akatimua mbio kuelekea nyumbani akiwa na furaha kubwa.

Siku moja Simba alipokuwa akizungukazunguka huko msituni akitafuta chakula, alinaswa na wavu mkubwa akawa hawezi kujinasua. Alijaribu kujirusha huku na kule lakini aliambulia patupu. Kwa bahati ya mtende, alitokeza Panya aliyekuwa akienda kwenye safari zake za kutafuta chakula kama kawaida. Alipomwona Simba alimkaribia na kumwuliza , "Je Simba **mwandani** wangu, kwa nini unalia jinsi hii?" Nimezongwa na wavu huu nisiweze kutoka kabisa, sijui hata nifanye nini." "Mimi nitakusaidia," alisema Panya. Simba aliangua kicheko tena na kuuliza ,"Nimeshindwa mimi mwenyewe niliye na nguvu nyingi, utaweza wewe kinyama dhaifu?"

"Simba, mimi **nina meno makali kama kijembe**. Nitaukata wavu haraka. Utaona tu. "Alisema Panya na kuanza kuutafuna ule wavu.

Muda si muda shughuli ilikuwa imekamilishwa na Simba kutoka. Tangu siku hiyo wakaendelea kuishi kwa masikilizano na urafiki mwema.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza, sababu ya Simba kuzunguka kote ilikuwa ni
A. kuwaua wanyama
B. kuwafukuza wanyama
C. kutembea katika safari
D. kutafuta chakula

**42.** Ni wazi kuwa
A. Simba alimla yule Panya
B. siku hiyo Simba alikula lishe yake
C. siku hiyo Simba alilala njaa
D. zamani simba na Panya walikuwa marafiki

**43.** **Magego** kulingana na mwandishi ni aina ya
A. chakula
B. meno
C. mlo
D. nafasi

**44.** Kucheka kwa Simba kulionyesha
A. alivyomdunisha Panya
B. alivyopendezwa na Panya
C. alivyoshangazwa na Panya
D. alivyompenda Panya

**45.** Juhudi za Simba za kujinasua kwenye wavu
A. hazikumfaa
B. zilimsaidia
C. zilimpa hasira
D. zilimrusharusha

**46.** "**Mwandani**" ni
A. Panya
B. rafiki
C. kilicho ndani
D. adui

**47.** Methali inayofaa kifungu hiki ni
A. mnyonge hana haki .
B. adui mpende.
C. akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.
D. mwenye nguvu mpishe.

**48.** Panya aliposema "**Nina meno makali kama kijembe**" Fani hii ya lugha inaitwa
A. methali
B. istiari
C. nahau
D. tashbihi

**49.** Panya alikata wavu ule
A. siku nzima
B. kwa muda mfupi sana
C. kwa saa nyingi
D. kabla ya jua kutua

**50.** Kama Panya asingepita karibu na ule wavu, bila shaka
A. Panya angekosa chakula siku hiyo
B. Simba angelala njaa
C. Simba angekufa siku hiyo
D. Panya angelala njaa

Compiled & supplied by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com